

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOKETI TAREHE  
08/02/2022 KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

- |                         |            |
|-------------------------|------------|
| 1. FRANCIS MAGHEMBE     | MWENYEKITI |
| 2. HONEST WILLIAM       | KATIBU     |
| 3. DR. MHAGAMA INNOCENT | MJUMBE     |
| 4. RAJAB BOGWA          | MJUMBE     |
| 5. APOLINARY SEIYA      | MJUMBE     |
| 6. ALLAN SAID           | MJUMBE     |

**WAALIKWA**

- |                   |                |
|-------------------|----------------|
| 1. TINGA A. TINGA | KAIMU MHANDISI |
| 2. GASPAR KALINGA | MWANASHERIA    |

**AGENDA ZILIZOJADILIWA**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUTHIBITISHA AGENDA
3. KUPITISHA NJIA YA UNUNUZI YA UJENZI WA JENGO LA HUDUMA YA DHARURA (EMD) KATIKA HOSPITALI YA MJI WA MAFINGA
4. KUFUNGA KIKAO

**AGENDA NA. 1: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 6:40 mchana kwa kuwakaribisha wajumbe wote nakutaka kuchangia mada zitakaziwasilishwa kwa ajili ya kuyatolea maamuzi ambayo yatasaidia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Halmashauri.

**AGENDA NA 2; KUTHIBITISHA AGENDA**

Wajumbe waliridhia agenda hizoziweze kujadiliwa.

**AGENDA NA. 3: KUPITISHA NJIA YA UNUNUZI YA UJENZI WA JENGO LA HUDUMA YA DHARURA (EMD) KATIKA HOSPITALI YA MJI WA MAFINGA**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imepokea fedha kiasi cha shilingi 300,000,000/= ikiwa ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la matibabu ya dharura katika hospitali ya Mji wa Mafinga.

Katibu aliwaelekeza wajumbe kwamba kutokana na kazi hii kutangazwa na kukosa mkandarasi mwenye vigezo wa kufanya kazi hiyo. Kwa kuzingatia Sheria ya manunuzi ya mwaka 2011 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016 kifungu namba 64 (5), Kitengo cha manunuzi kinapendekeza kazi hii ifanyike kwa mfumo wa Force Account. Pia katika utekelezaji wajumbe wakamati ya utekelezaji wa mradi

wanatakiwa kuzingatia Muongozo uliotolewa na PPRA, muongozo Na.PPRA:GL/05/2020/FA wa tarehe 22/05/2020.

**Maamuzi ya Bodi ya Zabuni**

Bodi ya zabuni iliridhia matumizi ya mfumo wa Force Account katika utekelezaji wa miradi tajwa hapo juu, na kusisitiza wajumbe wote wakamati watako chaguliwa kutekeleza mradi tajwa hapo juu wajengewe uwezo.

**AGENDA NA 4 : KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 7.16 na kuwashukuru wajumbe kwa michango yao pamoja na maoni waliyotoa kwa ajenda iliyowasilishwa.

**UMETHIBITISHWA**

Saini .....  
Mwenyekiti

Saini .....  
Katibu

Tarehe.....13/03/2022.....